**SEVENTH –DAY ADVENTIST CHURCH**
**SOUTH NYANZA CONFERENCE**
**NGULYATI ADVENTIST SECONDARY SCHOOL**
**P.O. BOX 104.**
**BARIADI- SIMIYU**
**Tel: Mkuu wa shule:+255719799331 Mhazini:+255768114850**
**Makamu mkuu wa shule: +255788 849 016 Mtaaluma: +255757 585 755**

**Kumb.No.NSS/FI/2024/01**
**19 /10/ 2023**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NGULYATI 2024.**

Kwa niaba ya Bodi na Uongozi wa shule, ninapenda kukupongeza kwa kuchaguliwa kujiunga katika shule hii . Hongera na karibu sana, Mungu akubariki.

Shule ya sekondari Ngulyati ni shule ya bweni na kutwa inayomilikiwa na Kanisa la Waadventista wa Sabato South Nyanza Conference yenye Kidato cha kwanza hadi cha nne iliyobobea katika kufundisha masomo ya **Sayansi**, **Sanaa** na **Biashara**

Shule hii haina ubaguzi wo wote kwa misingi ya kikabila, dini, rangi, itikadi au kijinsia. Watu wa kabila, dini, rangi, itikadi na jinsia zote huishi kwa pamoja kama ndugu na dada katika ushirikiano na upendano unaolenga kumkuza, kumlea na kumwendeleza Mwanafunzi katika nyanja kuu NNE za Maisha ambazo ni **KIAKILI, KIMWILI, KIROHO na KIJAMII.**

**MAHALI SHULE ILIPO:**

a) Shule ipo **kijiji cha Ngulyati, Halmashauri ya wilaya ya Bariadi mkoa wa Simiyu**. Shule iko takribani **kilomita 20** Magharibi mwa mji wa Bariadi katika Barabara itokayo Bariadi mjini kwenda Mwanza kupitia Ngulyati, Kasoli na Magu.
b) Kwa anayetoka nje ya Bariadi shuka stendi kuu ya mabasi ya mkoa wa Simiyu (Somanda-Bariadi) kisha panda magari ya kuja senta ya Ngulyati na ukifika tembea au panda pikipiki kuja shule ya sekondari Ngulyati.
c) Kwa anayetokea au kupitia mkoa wa Mwanza njoo mpaka Magu kuja Kasoli hadi senta ya Ngulyati kisha shuka na uje shuleni.
d) Kwa atakayetatanika na namna ya kufika shuleni piga namba za simu zilizo kwenye fomu hii hapo juu.

**MUHIMU:**

i) Siku ya kumtembelea mwanafunzi akiwa shuleni ni **Jumapili ya wiki ya mwisho** ya **Februari, Mei, Agosti na Oktoba** tu na si vinginevyo. Anayemtembelea ni mzazi/mlezi tu na haruhusiwi kumletea mwanafunzi chakula au kinywaji cha aina yoyote.
ii) Wastani wa kumruhusu mwanafunzi kuingia kidato kingine ni alama **41%**

**02. MAHITAJI YA MWANAFUNZI YA KUJA NAYO (SARE YA SHULE)**

**a)** Suruali/Sketi 02 nyeusi na shati 02 nyeupe mikono mifupi kwa ajili ya darasani.
**b)** Tai ndefu mbili(02) moja ni nyeusi na ya kijivu zitakayovaliwa na sare za darasani na matukio mengine
**c)** Suruali/Sketi mbili (02) rangi damu ya mzee kitambaa kizito sare nje ya madarasa.
**d)** Suruali/sketi ya kijivu mpauko na shati nyeupe mikono mirefu sare ya matukio maalumu mfano ibada.
**e)** Sweta rangi ya bluu halisi(siyo rangi ya bluu nyingine yoyote ile)
**f)** Viatu Jozi/Pair 01 au 02 vyeusi vya ngozi vya kamba wanafunzi wote, vyenye visigino vifupi na soksi pair 2 nyeupe (Soksi ziwe ndefu). Pia aje na Viatu vya wazi (Open shoes) nyeusi za kuvaa baada ya saa za madarasa.
**g)** T-Shirt ya michezo rangi ya bluu wanafunzi wote na bukta ya bluu kwa wavulana tu.
**h)** Wanafunzi wote wanatakiwa waje na Track Suit ya kijivu mpauko kwa ajili ya mchakamchaka, michezo na mazoezi mengine ya viungo.

**i)** Raba nyeusi (Wavulana); wasichana raba nyeupe na soksi bluu ndefu (wote).
**j)** Wavulana mkanda wa suruali mweusi usio na urembo wowote.
**k**) Hairuhusiwi (Ni marufuku) mwanafunzi kuonekana na nguo yeyote ya nyumbani akiwa shuleni.

**MUHIMU:**

*Suruali zote lazima ziwe za kitambaa si mtumba zenye malinda mawili na mfuko wa nyuma mmoja na ziwe na turn up(tanap). Upana wa suruali zote chini miguuni ni lazima kuanzia **inchi kumi na sita (16).** Suruali zenye mtindo wa kubana (Pistol style/Model) ni marufuku.Zingatia upana ulioelekezwa.
*Wasichana, **urefu wa sketi zote uwe kasoro nchi moja tu kufika kwenye kifundo cha mguu chini** na sketi zote ziwe na marinda 18 au zaidi**.**

## 03. MAHITAJI MENGINE YA MUHIMU YA KUJA NAYO SHULENI

a) Godoro futi mbili na nusu (2½) (Kama unatoka mbali yanapatikana pia senta ya Ngulyati).
b) Ream moja aina ya A4 (Kwa kila muhula)
c) Mfagio mmoja mgumu wa chelewa (hata senta ya Ngulyati wanauza)
d) Madaftari makubwa kuanzia 12 (Quire 3)
e) Dictionary.
f) Ndoo kuanzia mbili (02) ndogo za lita 10.
g) Sahani 01, Bakuli 01, Kikombe 01 (nusu lita) na kijiko kimoja (01)
h) Chandarua (mosquito net) bluu yenye pembe nne (4 x 6)
i) Shuka mbili (Pinki na Bluu) na blanketi (si lazima). Shuka nyingine tofauti ya hizi ni marufuku.
j) Kadi ya Bima ya afya (NHIF) kama anayo.
k) Mafaili mawili (moja kubwa la kutunzia mitihani (Box file) na moja dogo la kumbukumbu za mwanafunzi shuleni.
l) Sanduku la chuma (Trunk) la kutunzia vifaa vya mwanafunzi na kufuli zake
m) Torch(kurunzi) moja kwa matumizi binafsi
n) Jembe moja na mpini wake
o) Fyekeo (kwanja) moja
p) Dumu/galoni lita tano kwa ajili ya kutunzia maji ya kunywa
q) Unashauriwa kununua kitabu cha kiada angalau kimoja kwa kila somo ukiweza (Cha serikali cha sasa-TIE)

## 04. ADA NA MALIPO MENGINE MBALIMBALI

- **i)** **Karo ya Bweni ni T.Shs 1,400,000/= (Million moja laki nne tu)** kwa mwaka.
- **ii)** **Karo ya kutwa ni tsh. 1,050,000/= (milioni moja na elfu hamsini tu) kwa mwaka**
- **iii)** **Michango yote ilipwe muhula wa kwanza pamoja na ada ya muhula husika**
- **iv)** Karo hairudishwi kwa mwanafunzi atakayefukuzwa shule au atakayehama shule.
- **v)** Malipo yote hulipwa kabla mwanafunzi hajaripoti shuleni na stakabadhi za malipo ya benki (Bank pay slip) zote ziwasilishwe mara moja mwanafunzi anaporipoti shuleni.

MUHTASARI WA KARO NA MALIPO MENGINE MBALIMBALI.

| | HITAJI | KIDATO CHA I AU MGENI | KIDATO CHA II | KIDATO CHA III | KIDATO CHA IV |
|---|---|---|---|---|---|
| | **MUHULA WA KWANZA** | | | | |
| 1 | T-shirt 02 | 24,000/= | | | |
| 2 | Matibabu | 25,000/= | 25,000/= | 25,000/= | 25,000/= |
| 3 | Kitambulisho | 5,000/= | | | |
| 4 | Student handbook | 10,000/= | | | |
| 5 | Vitabu vya Kiroho | 40,000/= | 10,000 | 10,000 | 10,000 |
| 6 | Graduation (Mahafali) | 15,000/= | 15,000/= | 15,000/= | 40,000/= |
| 7 | Mock examinations | | 15,000/= | | 25,000/= |
| 8 | Mtihani wa Taifa | | 10,000/= | | 50,000/= |
| 9 | ZONE “A” Exams | | 15,000/= | | 25,000/= |
| 10 | Non-government exams | | 15,000/= | | 25,000/= |
| 11 | Maendeleo ya shule | 70,000/= | 70,000/= | 70,000/= | 70,000/= |
| 12 | Umiseta | 5,000 | 5,000 | 5,000 | 5,000/ |
| | **Jumla ndogo** | **194,000/=** | **180,000/=** | **125,000/=** | **275,000/=** |
| 13 | KARO | 700,000/= | 700,000/= | 700,000/= | 700,000/= |
| | **Jumla muhula wa kwanza** | **894,000/=** | **880,000/=** | **825,000/=** | **975,000/=** |
| | **MUHULA WA PILI** | | | | |
| 14 | KARO | **700,000/=** | **700,000/=** | **700,000/=** | **700,000/=** |
| | **Jumla kuu ya mwaka** | **1,594,000/=** | **1,580,000/=** | **1,525,000/=** | **1,675,000/=** |

Pesa zote za ada na michango mbalimbali zilipwe benki au kwa wakala wa Benk popote hapa nchini kupitia: kumbuka kuandika jina la mwanafunzi na kidato chake wakati wa malipo.

NMB A/C No: **3 0 5 1 0 0 0 4 8 1 5 (NGULYATI SECONDARY SCHOOL)**

**KUMBUKA:**

Hatupokei pesa taslimu shuleni. Lipa pesa yote kupitia Benki na kisha utuletee Risiti Original Benki ya pesa uliyolipa. **ANDIKA JINA LA MWANAFUNZI KWENYE RISITI YA BENKI** kama mlipaji.

**05. KUFUNGUA SHULE**

*Shule itafunguliwa **Jumapili** tarehe **07 Januari 2024 Karibu sana.**

ZAWADI N. MNGUMI
MKUU WA SHULE

**NGULYATI SECONDARY SCHOOL**
**SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE KAMA ZILIVYOWEKWA NA WIZARA YA ELIMU NA UONGOZI WA SHULE**

BANDIKA PICHA

**MAKOSA YATAKAYOMFUKUZISHA SHULE MWANAFUNZI**

1. Wizi
2. Uasherati, ubakaji, ushoga, ulawiti na usagaji au viashiria vingine vya ngono
3. Ulevi wa pombe, uvutaji sigara, utumiaji au uuzaji wa madawa yoyote ya kulevya
4. Kupigana, kupiga au kutukana mwanafunzi mwenzako, mtumishi wa shule au mtu yeyote.
5. Kuharibu mali ya umma au ya mtu yeyote
6. Kudharau Bendera ya Taifa, Picha za viongozi wa Taifa, Nembo ya Taifa, Wimbo wa Taifa au uongozi wa shule.
7. Kuoa au kuolewa
8. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani au nje ya shule
9. Kutoa, kushawishi au kudhamiria kwa kuchukua hatua za kutoa mimba
10. Kugoma,kuchochea na/au kuongoza au kuvuruga amani na usalama shuleni
11. Kukataa adhabu halali inayotolewa shuleni
12. Utoro wa siku tisini (90) mfululizo.
13. Makosa mengine ya jinai
14. Kumiliki simu na au kuwa na vielelezo vingine vya kuwa na simu kama charger, earphone, headphone, memory cards, MP3, power bank, laini ya simu na au kumiliki vifaa vya kieletroniki kama redio, kamera, flash disk n.k
15. Kumiliki silaha shuleni kama panga, mkuki, kisu, mkasi, rungu, bunduki au chochote chenye ncha kali.
16. Kutofanya kazi za darasani na au mtihani kwa makusudi.
17. Kutovaa sare za shule makusudi wakati wa kwenda likizo (nyumbani) au arudipo shuleni baada ya likizo
18. Kutoroka na kwenda nje ya shule na au kulala nje ya shule bila ruhusa ya mkuu wa shule.
19. Kutumia lugha chafu kwa viongozi au mtumishi yeyote wa shule
20. Kughushi nyaraka kwa lengo la kudanganya na au kuibia mtu, shule au taasisi nyingine au kwa nia nyingine yoyote ovu
21. Kunyoa kiduku (denge) au mitindo mingine ya kihuni.
22. Kufanya biashara yoyote shuleni
23. Kudharau misingi na kanuni ya kanisa la Waadventista wa Sabato ikiwemo uvunjaji wa Sabato, kutokuheshimu ibada za kila siku na au mikutano mingine ya kidini kwa mujibu wa ratiba ya shule.
24. Kufuga ndevu, nywele ndefu, kuvaa pete, mikufu, michoro au kupaka rangi sehemu zozote za mwili kama mdomo, kucha au kupaka rangi mywele(Curl kit)
25. Kuchungulia na au kuingia bweni la jinsia tofauti bila idhini/ruhusa maalumu toka uongozi wa shule.

**TAMKO LA MZAZI/MLEZI LA KUKUBALIANA NA SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE KAMA ZILIVYOWEKWA NA WIZARA YA ELIMU NA UONGOZI WA SHULE**

Mzazi/Mlezi unao wajibu wa kusaidiana na walimu na walezi wengine ili kumjenga mtoto/mwanafunzi kitabia, kinidhamu na kitaaluma. Baada ya kuzisoma na kuzielewa Sheria na Taratibu hizi za shule, tafadhali jaza sehemu hii hapa chini kuonyesha kukiri kukubaliana na Sheria hizi.

Mimi_______________________________________ Mzazi/Mlezi wa_____________________________________________
(Jina la mzazi/mlezi) (Jina la Mwanafunzi)

Nikiwa na akili zangu timamu, bila kulazimishwa, wala kushawishiwa na wala si kwa kutoelewa ninakiri kukubaliana na Sheria na Taratibu hizi za Shule. Sitakuwa na sababu ya kulalamika kwa hatua zitakazochukuliwa na Uongozi wa Shule ikiwa mtoto wangu atavunja mojawapo au baadhi ya sheria hizi.

________ __________ __________________ _________ ________________ ____________
(Mzazi-Saini) (Dole gumba (Tarehe) (Mwanafunzii-Saini) (Dole gumba) (Tarehe

Anuani ya Mzazi/Mlezi: ________________________________________________

S.L.P__________________________________________________________________

Namba ya Simu__________________________________________________ au___________________________________________

Kwa matatizo ya dharura na mawasiliano kwenye fomu hii hayapatikani Uongozi umwarifu nani ?

______________________________________ ______________________________
(Jina) (Uhusiano wake na mwanafunzi)

Anuani yake___________________________________________________________

S.L.P _________________________________________________________________

Simu: __________________________ Au ___________________________________

***MUHIMU*:** FOMU HII IKABIDHIWE KWA MAKAMU MKUU WA SHULE (MSAJIRI) SIKU YA KURIPOTI SHULE.

SEVENTH –DAY ADVENTIST CHURCH
SOUTH NYANZA CONFERENCE
NGULYATI SECONDARY SCHOOL
P.O. BOX 104
BARIADI- SIMIYU
Tel: Mkuu wa shule:+255719799331 Mhazini:+255768114850
Makamu mkuu wa shule: +255788 849 016 Mtaaluma: +255757 585 755

## MEDICAL EXAMINATION FORM

**NAME:** ________________________ **AGE:**________ **SEX:**_______

**PART A**

**To the Medical Officer,**

**Please examine of the above named as to his/her physical and mental fitness for joining Secondary School. The examination should include the following categories (I -IV) each category or sub-category of which, will render the applicant ineligible in each of a defect.**

**Pregnancy (Category III) will also render girl candidate ineligible.**

**I.** a) **Eye-sight**______________________
b) **Hearing**______________________
c) **Limbs**______________________
d) **Speech**______________________
e) **Venereal disease**______________________
f) **Leprosy disease**______________________
g) **Epilepsy**______________________

**II.** **Neuroses**______________________

**III.** **Pregnancy** ______________________

**IV.** **Other serious diseases** ______________________

%%%%%%%%%%%%%%%%%%%%%%%%%%%%%%%%%%%%%%%

**PART B**

**MEDICAL CERTIFICATION**

**(To be completed by a medical Officer)**

**I have examined the above named and consider that he/she is physically fit/unfit and mentally fit/unfit for a full time Secondary Education course.**

**DOCTOR'S NAME:** ______________________ **SIGNATURE:**____________

**DATE:** ______________________ **OFFICIAL STAMP:** ______________________

***MUHIMU***: FOMU HII IKABIDHIWE KWA MAKAMU MKUU WA SHULE (MSAJIRI) SIKU YA KURIPOTI SHULENI

**School Motto:** *"Education for a Difference"*